Fanyeni Kiume

na

J D Logan

Fanyeni Kiume

na

J D Logan

Novemba 5, 2011

Fanyeni Kiume

"*Kesheni, simameni imara katika Imani, fanyeni kiume mkawe hodari.*" (1 Kor. 16:13)

Maneno haya si ya kipekee kwa mtume Paulo au kwa swala hilo, kwa Biblia. Katika njia nyingi na mifumo tofauti zimerudiwa mara nyingi kwa wanajeshi (kiroho na kiupole) kupitia katika kurasa zote za historia.

Wanajeshi wa zamani walitiwa moyo "Kusimama kila mtu katika nafasi yake na asiruke kama ndege aliyetishiwa" katika uso wa adui.

Katika mazingira ya historia yetu wenyewe, mwanajeshi mtaifa walimsihi kuto "kupiga bunduki hadi atakapoona weupe wa macho yao". Inachukua ujasiri wa upendeleo kusimama katika uso wa adui ukiwa umeegama katika maangamizi ya mwingine.

Tunawadai hao wakoloni wa zamani deni la ujasiri wa kusimama katika ardhi yao kwa ujasiri; "*Walifanya kiume.*"

Hii yote inatuongoza wapi? Kawaida sisi, kama Wakristo, hatupaswi kupigana vita vya kiroho na maadui zetu. 2 Kor. 10:4, "*…silaha za vita vyetu si za kimwili…*".

Lakini Wakristo WANA vita vya kupigana. 1 Tim. 1:18, "*Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri.*" Pia kumbuka 1 Tim. 6:12, "*Piga vita vile vizuri vya imani…*".

Vita vyetu kama Wakristo, vinahusisha, "…(silaha) *Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.*" (2 Kor. 10:4-5).

Hili ni onyo la ulimwengu wote; hata maadui za Mungu huitumia. Kama ilivyoandikwa katika 1 Sam. 4:9, Wafilisti, wadhaifu, watu walioabudu sanamu waliokuwa katika vita na Israeli, wakasikia mlio mkubwa kutoka katika kambi ya Waisraeli (sanduku la agano limerudishwa Israeli) na, kuogopeshwa, walitiwa moyo kuwa "*Iweni hodari, na kufanya kiume enyi Wafilisti, msije mkawa watumwa wa Waebrania, kama wao walivyokuwa watumwa wenu; fanyeni kiume mkapigane nao.*"

Kwa ufupi, maneno yanamanisha sifa zote hasa ukizingatia *kiume*.

Lakini kwa matumizi gani na kwa kusudi gani maandiko yanatoa sifa hizi?

Tuko Vitani

2 Tim. 2:3, "*Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia ili ampendeze yeye aliyemwandika ili awe askari.*"

Hatupaswi kutiwa upofu kwa ukweli kwamba vita vya aina yo yote, ni jukumu ambalo linapaswa kupiganwa kwa shauku, ili ushinde. (Ni nani anayepigana katika vita ili ashindwe?) ili upigane vita dhabiti, mtu lazima atumie silaha kama kinga yake kuangamiza zile za adui: pia kujikinga mwenyewe kutokana na kukabiliana na adui.

Jaribu mambo Yote

1 Thes. 5:21, "*Jaribuni mambo yote lishikeni lililo jema;*" Efe. 5:10, "*Mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.*" Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"

Tukijaribu kuleta "mizigo" yetu ya dunia tunapoingia kanisani, *hatufanyi upya* nia zetu. Tutawezaje kujua "mema, yanayokubalika na mapenzi ya Mungu yaliyo kamilifu"?

Lakini, kama tukiacha yaliyojaa katika ulimwengu na yote yanayoshikamana nayo, tutakuwa tumefanya upya nia zetu na tutaanza *kujaribu* mambo yote.

Baada ya kufanya hivyo, tumechukua tu kinga (kabili) silaha zilizotolewa na "kiongozi" wa vita. Hatuna njia nyingine yo yote ya kukabiliana na maadui zetu. Lakini tunapaswa kupigana kwa njia gani? Na mfumo wetu unatakiwa uweje?

Silaha Zetu Ni Za Kiroho

Paulo anatuambia "*...nia ya mwili ni mauti…nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu; …haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.*" (Rum. 8:6-7). Kama sisi tulio wa rohoni tunajaribu kujaribu mambo yote kwa nia ya mwili, hatuwezi kufanikiwa: hatutaweza kupigana vita vya kiroho. "*Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.*" (Rum. 8:8).

Lazima tuwe na Msimamo

Paulo analinganisha wakati alipokuwa na majaribu makali, marafiki zake wote walimkimbia; alisimama peke yake mbele ya kiongozi wa Rumi Nero (uwezekano) katika mahakama mwenyewe. 2 Tim. 4:16, "*Katika jawabu langu la kwanza hakuna mtu aliyesimama upande wangu, bali wote waliniacha…*" Ni mara ngapi inaonekana kuwa tunasimama peke yetu katika maisha yetu?

Fanyeni Kiume

Paulo hakushtuka. Alijua kuwa wengi wetu wanashindwa kutambua leo; kwamba "Bwana na wewe mwenyewe ni wawili walio wengi."

2 Tim. 4:17, "*Lakini Bwana alisimama pamoja nami kanitia nguvu… nami nikaokolewa katika kinywa cha simba.*" Kama sisi ni watiifu katika mapenzi ya Mungu katika shughuli zetu zote, hatatuacha. 2 Tim. 4:18, "*…Bwana ataniokoa na kila neno baya, na kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni…*"

Inachukua ujasiri ili uwe na msimamo katika uso wa adui na pingamizi yaw engine lakini ujasiri ni wa kwanza "Wema wa Mkristo" tunayoambiwa "kuongeza katika imani yetu". Petro anatuambia katika 2 Pet. 1:5, "*…katika imani yenu tieni na wema…*" wema katika mtazamo wake ni ujasiri. Hatupaswi kushindwa kupigana "vita vizuri" wakatika umuhimu akituijia. Kufanya hivyo tutakuwa waoga.

Wakati mwingi sana, tunakabiliwa na changamoto yakiwa yamelenga katika imani yetu na tunaogopa katika majukumu yetu ya vita. Kama tuna silaha zote, pamoja na "upanga wa roho" na "silaha zote za Mungu", je tunaogopa nini?

Silaha zetu zitakuwa somo la wakati ujao, ikimalizika lenyewe.

Hivyo ndugu, hebu na "tusimame kila mmoja kwa nafasi yake" wito unapokuja tusiache uwanja kwa adui! Kwa kufanya hivyo, tutakuwa *tutakuwa tunafanya sisi wenyewe kiume*."

Katika kinga ya ukweli na upendo wa ndugu,

Ndugu yenu katika Kristo,

J. D. Logan